

PROGRAMU YA KISIKI HAI MKOA WA DODOMA 2017 – 2022

WILAYA YA MPWAPWA

MCHAKATO WA KUCHAGUA WAWEZESHAJI WANNE KILA KIJIJI

Utangulizi

Lengo: Kuwezesha wilaya ya Mpwapwa itekeleze kwa ufanisi na ifanikiwe kufikia malengo yake ya kuyakomboa mazingira.

Madhumuni

1. Kuhakikisha wanapatikana wawezeshaji hodari na walio na dhamana ya wakulima wanaojulikana walio watuma kupitia serikali zao za vijiji.
2. Kutimiza dhamana. Wilaya hizi tatu na LEAD Foundation wanabeba dhamana ya kuwezesha wilaya zilizosalia za Mkoa wa Dodoma na Mikoa mingine kame ya Tanzania kufikiwa na programu hii.
3. Kuthamini motisha kwa wawezeshaji. LEAD Foundation na washirika wenza wake wamepanga kutoa motisha kwa wawezeshaji, kama alivyotaja Meneja wa Programu. Wawezeshaji wawe mawakili wema.
4. Namna ya Wilaya ya Mpwapwa na LEAD Foundation kutimiza dhamana hiyo ni kuhakikisha wanapatikana wawezeshaji waaminifu, wabunifu, wenyewe juhudhi na moyo wa kujituma kutokana na uchungu wa uharibifu wa mazingira yao.
5. **Wawezeshaji hawa watahitaji kufuatiliwa kwa karibu na mabalozi wao, serikali ya kijiji akiwemo Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata, Diwani, na viongozi wa wilaya.**
6. Mchakato huu ni matokeo ya tuliyojifunza Wilaya ya Kongwa. Siyo vizuri kurudia makosa.

Mchakato:

1. Tunashauri mara baada ya warsha hii ya Wilaya, kuwe na kikao ngazi ya Kata, wakiwemo wenyeviti na watendaji wa kata, kuifikisha Programu hii na utaratibu wa kuteua wawezeshaji wa vijiji.
2. Baada ya kikao cha kata, Mwenyekiti na Mtendaji wa Kijiji waitishe mkutano wa serikali ya kijiji, ukiwa na Mabalozi wote, kuchagua wawezeshaji wao.
3. Kila mwezeshaji anatazamiwa awezeshe kaya kati ya 150 hadi 200.
4. **Hivyo, kila mwezeshaji aliyeuleliwa apewe majina ya viongozi wa kaya hizo, na mabalozi wake.**

5. Utaratibu huu unampa nguvu na lengo maalum mwezeshaji kwa kuja watu anaokwenda kuwawezesha wanafahamika.
6. Wawezeshaji watakaporudi kutoka kwenye mafunzo wata ripoti kwa serikali ya kijiji, itakayoitisha mkutano wa kijiji kuwapokea wahitimu wao na kuwapa nafasi ya kuelezea mpango wao wa utekelezaji wa kisiki hai watakaokuja nao. Kisha wawezeshaji wataanza shughuli yao kwa kaya walizopangiwa.
7. Taarifa ya kila miezi mitatu ya mwezeshaji, yenyе sahihi ya Mwenyekiti na Mtendaji wa Kijiji, ipelekwe kwa Meneja wa Programu, nakala kwa Mtendaji wa Kata.
8. Tunashauri pia, Mtendaji wa Kata, katika taarifa yake kwenye Kikao cha Kata, iwemo taarifa ya maendeleo ya Kisiki Hai katika Kata.

7. Tarehe za Mafunzo

Kufika: 19 Agosti 2019, Saa 7.00 mchana

Kuondoka: 24 Agosti 2018, asubuhi.

Mahali: Chuo cha Mifugo (LITA), Kikombo, Mpwapwa.

PROGRAMU YA KISIKI HAI MKOA WA DODOMA

TAARIFA YA UTEUZI WA WAWEZESHAJI WA KIJINI

Jina la Kijiji..... Kata.....

Tarafa..... Wilaya.....

Kikao cha Kata kilifanyika Tarehe.....

Uteuzi ulifanyika kwenye Kikao cha Serikali ya Kijiji, Tarehe.....

Mwenyekiti wa Kijiji:

Jina..... Sahihi..... Tarehe.....

Mtendaji wa Kijiji:

Jina..... Sahihi..... Tarehe.....

WALIOTEULIWA

| | | JINSIA | UMRI | ELIMU YAKE | JIBU “NDIYO” AU “HAPANA” PANAPOHUSIKA | | | |
|---|----------------------|--------|--------------------|------------------|---------------------------------------|----------------|----------------|-----------------------|
| | JINA LA ALIYETEULIWA | ME/KE | TAREHE YA KUZALIWA | TAJA DARASA LAKE | ELIMU YA KISIKI HAI | SHAMBA BINAFSI | KAZI ZA KIJINI | UONGOZI WOWOTE KIJINI |
| 1 | | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | | |

UTHIBITISHO: AFISA MTENDAJI WA KATA

Jina..... Sahihi..... Tarehe.....



UHAKIKI WA LEAD FOUNDATION: MENEJA WA TOT

Wasiothibitishwa:

1.Sababu:
2.Sababu:.....
3.Sababu:.....

Jina.....Sahihi:.....Tarehe.....

MUHIMU:

1. **Kufika:** 19/8/18(Saa 7 mchana)
2. **Kuondoka:** 24/8/18 asubuhi.
3. **Mahali:** Chuo cha Mifugo(LITA) Kikombo, Mpwapwa.
4. **Uhakiki:** Shirika litafanya uhakiki mara mwezeshaji aliyeulewa anapofika.
 - Mwezeshaji ambaye hatakidhi vigezo vilivyotolewa, na ambaye hatakuja na orodha ya wakuu wa kaya alizopangiwa, na majina ya Mabalozi wa kaya hiso, hatapokelewa kwenye mafunzo.
 - Mwezeshaji huyo hatarudishiwa nauli na wala hatapewa nauli ya kurudia nyumbani.

TAFADHALI UTEUZI UFANYWE KWA MAKINI SANA.